

JIMBO KUU LA DAR ES SAALAM

MWEZI WA MALAIKA WAKUU.

NOVENA YA KUTUKUKA KWA MSALABA

KUANZIA TAREHE 6- 14/9/2020

K. Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu

W. Amina.

K. Bwana wa utukufu alipigiliwa misumali juu ya Msalaba

W. kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu – Wimbo wa msalaba

Utaratibu – Baba yetu x 3

1. Sala – salamu maria x 3
2. Atukuzwe x 3
3. Somo la siku
4. Novena ya siku husika
5. Sali Rozari ya Mt Mikael
6. Litania ya msalaba

SALA ZA SIKU

SIKU YA KWANZA: Utuwezeshe uheshimu wetu wa Msalaba utusaidie kuwa wenye upendo zaidi. Hivyo tuweza kuwapenda jirani zetu na kuondokana na hasira, kutoaminiana au kuwa na kinyongo katika mioyo.

- Somo – Mt. 18:15 - 20

SIKU PILI: Utufundishe kupokea mateso, tuyaunganishe na Msalaba wako utupe neema ya kuamini kuwa una uwezo ya kufanya jema hata katika hali mbaya kabisa.

- Somo Lk. 6:6 -11

SIKU YA TATU: Utusaidie kubeba maumivu ya maisha yetu ya kila siku utuvuvie tusikimbie maumivu na mateso, lakini kuyakubali na kuuishi msalaba wako kama uthibitisho wa upendo wetu kwako.

- Mt. 1:1 – 6, 18 – 23 – (Kuzaliwa Bikira Maria)

SIKU YA NNE: Uwe nasi, ili tuweze kupambana na majaribu yetu kwa ushujaa. Kwani twafahamu kwamba kwa njia yako, tunaweza kujifunza jema kutokana na majaribu hayo.

- Lk. 6:20 -26 – (Peter Clavery)

SIKU YA TANO: Utufundishe kuwa wavumilivu tunapokutana na matukano na maneno makalai ya wale wasiotupenda. Utuwezeshe kuwajibu kwa ukimya na utupe neema ya kuwaombea ili tuweze kukusaidia katika kuukomboa ulimwengu.

- Lk.6: 27 - 38

SIKU YA SITA: Utupe neema tusikate tama katika nyakati za mateso utusaidie kubeba misalaba yetu kwa ujasiri na kwa utu, hivyo kwamba hata tukiwa katika kilindi cha maumivu, tuweze kuwa msaada kwa wengine.

- Lk. 6: 3g - 42

SIKU YA SABA: Utusaidie kuepukana na tabia ya ujeuri, kukandamiza au kuwaonea wengine. Utupe moyo wa kupenda kutumikiana na kushindana katika wema na upole.

- Lk. 6:43-4g (Jina Takatifu la Maria)

SIKU YA NANE: Tufundishe kukubali mazingira na hali ambazo zipo nje ya uwezo wetu na kuzibeba kama wee ulivyobeba Msalaba wako mpaka Kalvari

- Mt. 18:21 - 35

SIKU YA TISA: Utujalie moyo wa ujakazi ili kwamba tuweze kuwasaidia wanaoteseka karibu nasi, Kwani tunafahamu kwamba tunapomsaidia aliyetelekezwa na mhitaji, kwa hakika twakutumikia wewe.

- Yh. 3:13 – 17 –(Kutukuka kwa Msalaba)

ZABURI YA KIITIKIZANO: (Zab 116:1-9)

Ant. Ee Mungu, umeokoa maisha yangu na kifo.

Nampenda Bwana kwa kuwa anaisikiliza Sauti yangu na Dua zangu maana amenitegea sikio lake, Kwa hiyo nitamwita siku zangu zote.

- Mat. 11: 27 – 30.

Imeandaliwa

Crispin T. Meela

0784 – 140199 – 0756 140199

(crismeela@gmail.com)